

VIGEZO VYA KUWAPATA WASHIRIKI WA MAONESHU YA NGUVU KAZI/JUA KALI YA AFRIKA MASHARIKI

Ili kupata wajasiriamali mahiri watakaoshiriki Maonesho ya Nguvu Kazi/ Jua Kali ya Afrika Mashariki vigezo vifuatavyo vitakavyotumika kuchagua washiriki:

1. Mshiriki mwenye kuzalisha bidhaa zenye ubora na kukidhi viwango vinavyokubalika kibiashara na watakaotoa sura halisi ya bidhaa zinazotengenezwa Tanzania hususan katika Mkoa husika;
2. Mshiriki awe na vipeperushi na kadi ya utambulisho wa bidhaa (business cards) kama nyenzo muhimu ya kutangaza bidhaa na kutafuta masoko;
3. Mshiriki awe na bidhaa za ubunifu wa hali ya juu, kipaumbele kikiwa ni bidhaa zinazotokana na ngozi na mazao ya ngozi, nguo pamoja na bidhaa za kilimo zilizosindikwa, mifugo, Bahari, viungo (spices) na urembo;
4. Mshiriki awe na cheti cha uasili wa bidhaa (Certificate of origin) kinachotolewa na TCCIA na ZCCIA kwa upande wa Zanzibar;
5. Mshiriki awe na vifungashio vizuri vya bidhaa yake vinavyokubalika kimazingira;
6. Mshiriki awe tayari kujaza dodoso la taarifa za maendeleo ya biashara yake wakati wa Maonesho kama itakavyotakiwa na kurejesha dodoso kwa waratibu wa maonesho;
7. Mshiriki awe na uwezo wa kujihudumia na kujigharamia kwa muda wote wa Maonesho; na
8. Mshiriki awe na Hati ya kusafiria.

Mambo ya kuzingatia wakati wa kujaza fomu:-

1. Kila mjasiriamali anayekusudia kushiriki atatakiwa:
 - i. Kujaza fomu za ushiriki ambazo zinapatikana katika Ofisi za Makatibu Tawala wa Mikoa na Wakurugenzi wa Halmashauri/Manispaa Tanzania Bara;
 - ii. Kujaza fomu za tathmini ambazo zitapatikana wakati wa maonesho na zitajazwa kwa maelekezo yatakatolewa
2. Mawasiliano kati ya wajasiriamali washiriki na Sekretariet ya Maonesho yafanyike kupitia viongozi wa Serikali na Vyama/Mitandao ya Wajasiriamali.

